

Rita F. Kilua ni Mhandisi aliyesajiliwa na Bodi ya Wahandisi Tanzania (ERB), mwenye Shahada ya kwanza ya Usimamizi wa Ujenzi wa miradi (*Construction Management*) kutoka Chuo Kikuu cha Kharkov cha nchini Ukraine. Pia ana Shahada ya Uzamili katika usimamizi wa Rasilimali za Maji kutoka Chuo Kikuu cha UNESCO-IHE, Delftn cha chini Uhlanzi.

Mhandisi Rita F. Kilua alikuwa anafanya kazi katika Idara ya Maji Vijijini kabla ya kuhamia Idara ya Huduma za Ubora wa Maji mwezi Novemba, 2018. Aidha, alifanya kama Fundi Mchundo (Ajira ya kwanza) Idara ya Haidrolojia - Maji Ubungo.